



Aina ya Miti Toleo TTS 5

Mjunju au Mkonga *Balanites aegyptiaca*, (Family Moraceae)

Mjunju wa aina ya *B. aegyptiaca* ni mmea usio wa kina kirefu na wenye miiba, na matawi hupukutika wakati wa kiangazi. Mmea huu hukua polepole na huweza kuishi hadi zaidi ya miaka 100. Aina ya mkonga huu huhimili viwango vya joto jingi hivyobasi hufaa sana katika nchi za hari hasa mahali pa ukame. Mmea huu ni maarufu katika kuangamiza wadudu. Matunda yaliyopondwa hutayarisha dawa inayoangamiza konokono wanaoleta ugonjwa wa kichocho (*Schistosomiasis*) na pia funza wa maji wanaosababisha ugonjwa wa Guinea worm disease.

Majina mengine: *Ximenia aegyptiaca*

Majina ya kawaida: Desert date, myrobolan, heglig, arraronyit, adhto, tiborak, ol-ngoswa, soapberry tree, Ndimu-mwitu, Baddan, Kilului, Mulului, oingoswa, Tuyunwa, othoo, mkonga, mtende, mwambangoma.

Maenezi: Mjunju huu umesambaa katika sehemu nyingi za Afrika karibu na Sahara, na hudhaniwa kutokea katika bonde la mto Nile. Mmea huu ni maarufu katika Afrika ya Kaskazini, na pia katika sehemu kame za Afrika kama Katanga kusini mwa Tanzania. Mmea huu pia ni maarufu nchini Israeli sehemu kame za Pakistan, India na Arabia.

Mazingira

Mvua: 200-900mm.

Kiwango cha joto: hadi 40°C.

Muinuko: 0-2000m.

Aina ya mchanga: Mchanga mweusi wa tope na hata mchanga wa changarawe au ule unaoadhiriwa na mafuriko. Mmea huu hautakidhi viwango vya maji kupita kiasi au mafuriko na hali kadhalika hautakidhi viwango vya chumvi.



Picha: Henrik Keiding
Forest & Landscape Denmark

Maumbile

Urefu: Hufikia 10-20m

Urefu wa shina: 45cm.

Maua: Maua ya rangi ya kijani kibichi hadi manjano huonekana mwezi wa Aprili kabla ya mvua nyingi na mduara wake ni 1cm. Maua huonekana kwenye chana moja au tano.

Matunda: Matunda ni kama yale ya mkonga wa kawaida, na hukomaa na kuanguka mwezi wa Desemba hadi Januari. Tunda la mviringo ni la uzito wa 10-15g lenye umbo kama *ndimu*.

Matumizi

Matumizi ya maana: Mmea huu ni maarufu kama lishe kwa mifugo hasa mbuzi, kondoo, ng'ombe na ngamia. Matunda yake hutayarisha dawa ya kukabili minyoo na konokono, hivyo basi hutumiwa kusafisha maji ya kunywa ili kuua viini. Dawa hii hutumiwa kuua samaki wanaoweza kutumiwa kama chakula.

Mmea huu hutoa kuni isiyo na mwoshi mwingi hivyo basi hufaa kwa matumizi ya nyumbani.

Matumizi mengine: Sehemu zote za mmea hutumiwa katika viwanda vya kutayarisha madawa na pia matunda ni chakula cha binadamu.

Mazao: Matunda 10,000 kwa kila mti; kwa kila mwaka.

Maelezo ya upanzi

Jamii hii ya mtende yaweza kupandwa kwa kutumia mbegu au vipandikizi.

Utaratibu wa kupanda: Lowesha mbegu kwa saa 24 katika joto la kawaida. Baada ya kuchuna mbegu kutoka kwa mti, mbegu hizo zaweza kuhifadhiwa hadi mwaka 1.

Kupanda: Iwapo unatumia mbegu, panda baada ya kiangazi. Mbegu zipandwe huku sehemu ya kutokea shina ikiangalia chini kisha kufunika kwa mchanga.

Utunzaji: Tunza mimea michanga ili isitafunwe na wanyama kwa hadi miaka mitatu kwa sababu ya ukuaji polepole. Palilia mara kwa mara ili kuondoa ushindani usiofaa.

Mengine

Magonjwa na wadudu: Mbegu hushambuliwa na wadudu wa mpekecha.

Upungufu: Mmea huu hukua polepole, hivyo basi utunzaji huhitajika kwa hadi miaka mitatu.

Tafsiri na: **Patrick Bunyali Kamoyani**

Tel +254-0721 612 607

Email: pbkamoyani@excite.com or pbkamoyani@lycos.co.uk

**Centre For Natural Resource Management, Advocacy And Marketing
(Cream)**

P.O Box 1427, 50300-Maragoli, Kenya.

E-mail: cream-creamorg@excite.com

Produced by the Tropical Advisory Service, June 2000

HDRA-Kwa huduma za Kilimo hai, Ryton Organic Gardens Coventry, CV8 3LG, UK. Simu +44 (0) 24 7630 3517 kipepesi +44 (0) 24 7663 9229 Barua-pepe ove-enquiry@hdra.org.uk
Mtandao: <http://www.hdra.org.uk>

Makala haya ni mkusanyiko wa utafiti wa kisayansi na maarifa ya kilimo hai. Maelezo ya ziada kuhusu mbinu za kilimo hai yaweza kupatikana kutoka kwa HDRA. Waweza kunakili makala haya kwa sababu zisizo za kifaida.